



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO  
BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA)



TAARIFA KWA UMMA

KUFUNGIWA KWA MSANII OSCAR JOHN LELO (WHOZU), KUTOKUFANYA  
KAZI ZA SANAA KWA MIEZI SITA KWA SABABU YA VIDEO YA WIMBO  
“AMEYATIMBA”.

**04 Novemba, 2023.**

Baraza la Sanaa la Taifa kupitia Sheria Na. 23 ya Mwaka 1984 na Marekebisho yake ya Mwaka 2019 ambayo inatoa Mamlaka kwa Baraza kusimamia Maadili ya msingi kwenye Sekta ya Sanaa kwa **Kanuni ya 25(1)-(8)** ya Kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa za Mwaka 2018.

Mnamo tarehe 02 Novemba, 2023 Mwanamuziki anayetambulika kwa jina la kisanii “Whozu” alichapisha video ya wimbo “Ameyatimba” akiwashirikisha wasanii wenzake “Mbosso” na “Bill Nass” wenye maudhui yanayokiuka kanuni za maadili kutokana na kuwepo ishara ya vitendo vinavyoashiria matusi kinyume na **Kanuni ya 25(6) (j)** pamoja na vitendo ya unyanyasaji, ukatili na udhalilisha wa utu wa mwanamke kinyume na **Kanuni ya 25(6)-(f)**.

Msanii huyu ameshaonywa mara mbili na kutozwa faini mara moja huko nyuma kwa kukiuka taratibu za kuzingatia maadili katika kazi za Sanaa lakini bado ameendelea kupuuza. Baraza limefanya uamuzi ufuatao;

- i. Limemtaka kushusha mara moja video ya wimbo huo kwenye *digital platform* zote
- ii. Limemtoza faini ya Shilingi Milioni tatu (3,000,000/=), (**Kanuni ya 64 (1)b**)
- iii. Limemfungia kujishughulisha na kazi za **Sanaa kwa muda wa Miezi 6**, (**kanuni ya 64 (1)d**) kuanzia leo tarehe 4 Novemba, 2023.

Aidha, wasanii **Mbosso na Billnass** wametoza faini ya milioni tatu (3,000,000) kila mmoja na kufungiwa kutokujishughulisha na kazi za Sanaa kwa muda wa **Miezi Mitatu** kuanzia tar. 4 Novemba, 2023.

Baraza limeshatoa na kuzindua mwongozo wa maadili katika kazi za sanaa ambao unapatikana katika tovuti yetu [www.basata.go.tz](http://www.basata.go.tz). Hivyo ni jukumu la kila msanii na mdau wa Sanaa kuzingatia maadili katika kazi za Sanaa.

Imetolewa na,



Dkt. Kedmon Mapana,  
Katibu Mtendaji,  
**Baraza la Sanaa la Taifa**